TANGAZO LA SERIKALI NA. 168 la tarehe 10/3/2023

SHERIA YA MAHAKAMA ZA MAHAKIMU,
(SURA YA 11)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 71(1))*

KANUNI ZA MAWAKILI NA WAENDESHA MASHTAKA KATIKA MAHAKAMA ZA MWANZO ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UANZISHAJI, UWAKILISHI NA UTARATIBU

4. Desturi na taratibu.
5. Notisi ya uwakilishi.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA JUMLA

6. Uahirishaji wa mashauri.
7. Mavazi.
8. Waraka wa utambulisho.
9. Ukadiriaji gharama.

JEDWALI

*Tangazo la Serikali Na. 168 (Linaendelea)*

SHERIA YA MAHAKAMA ZA MAHAKIMU,
(SURA YA 11)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 71(1))*

## KANUNI ZA MAWAKILI NA WAENDESHA MASHTAKA KATIKA MAHAKAMA ZA MWANZO ZA MWAKA 2022

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mawakili na Waendesha Mashtaka katika Mahakama za Mwanzo za mwaka 2022.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kusimamia mawakili na waendesha mashtaka katika mahakama za mwanzo.

Tafsiri
Sura ya 342

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vingenevyo-

"wakili" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya kifungu cha 2 cha Sheria ya Mawakili na inajumuisha watu waliotajwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hiyo;

Sura ya 430

"mahakama" maana yake ni mahakama ya mwanzo;

"Mkurugenzi wa Mashtaka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

Sura ya 430

"hakimu" maana yake ni hakimu mkazi anayesilikiza mashauri katika mahakama; na

"mwendesha mashtaka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

### SEHEMU YA PILI
### UANZISHAJI, UWAKILISHI NA UTARATIBU

Desturi na taratibu

4. Namna ya kufungua mashauri, desturi na taratibu za mahakama katika masuala yanayowahusisha mawakili na waendesha mashtaka zitakuwa kwa mujibu wa sheria zinazoongoza desturi na taratibu zinazotumika katika mahakama za mwanzo.

Notisi na ahadi ya uwakilishi

5.-(1) Wakili anayekusudia kumwakilisha mhusika yeyote katika mahakama atatoa taarifa na kuweka ahadi kwa maandishi mahakamani kwamba, ana maelekezo kamili na atahudhuria mahakamani kila mara shauri litakapotajwa au kusikilizwa.

(2) Baada ya kupokea taarifa na ahadi ya wakili chini ya kanuni ndogo ya (1), mahakama itajiridhisha iwapo wakili huyo ameajiriwa kumuwakilisha mhusika.

(3) Notisi na ahadi chini ya kanuni ndogo ya (1), vitakuwa kadiri itakavyowezekana, kama ilivyoanishwa katika Fomu A kwenye Jedwali la Kanuni hizi.

(4) Iwapo Mkurugenzi wa Mashtaka au mtu yeyote aliye chini yake ataona kuwa kuna ulazima wa shauri kuendeshwa na mwendesha mashtaka, ataijulisha na kuiahidi mahakama kwa maandishi kuwa, mwendesha mashtaka atahudhuria mahakamani wakati wowote wa kuendesha shauri hilo kama inavyoanishwa katika Fomu B kwenye Jedwali la Kanuni hizi.

(5) Wahusika wote katika shauri watapewa au kujulishwa juu ya notisi chini ya kanuni hii ndani ya wakati unaofaa kabla ya wakili au mwendesha mashtaka kuhudhuria kwa mara ya kwanza mahakamani.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA JUMLA

Uahirishaji wa mashauri

6.-(1) Usikilizaji wa shauri utakapoanza, utaendelea hadi mashahidi wote waliohudhuria mahakamani siku hiyo watakapotoa ushahidi, isipokuwa kama, kwa sababu zitakazoandikwa katika mwenendo wa shauri, mahakama inaona kuna umuhimu kuahirisha usikilizaji wa shauri hilo hadi siku nyingine.

(2) Wakili au mwendesha mashtaka kuhudhuria katika mahakama nyingine au baraza haitakuwa sababu ya kuahirisha shauri.

(3) Endapo wakili au mwendesha mashtaka ameshindwa kuhudhuria mahakamani kwa sababu ya kuhudhuria kwake katika mahakama nyingine au baraza, mahakama itamtaka mhusika kuendelea na shauri yeye mwenyewe na akikataa kuendelea au kama hayupo, mahakama itachukulia kwamba mhusika huyo ameshindwa kuhudhuria mahakamani na madhara ya kutokuhudhuria yatatumika.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2), endapo wakili au mwendesha mashtaka hajahudhuria mahakamani au ameomba ahirisho kwa sababu ya ugonjwa au sababu nyingine yoyote, mahakama haitakubali ombi hilo isipokuwa kama imejiridhisha kuwa wakili au mwendesha mashtaka ni mgonjwa au kwa sababu nyingine yoyote, hawezi kuhudhuria, au ikiwa amehudhuria, hawezi kuendelea, na mhusika anayeomba ahirisho hawezi kuendelea mwenyewe kwa sababu zinazofaa na asingeweza kuajiri wakili au kupata mwendesha mashtaka mwingine ndani ya muda.

Mavazi
T S Na. 118 la Mwaka 2018

7. Masharti ya Kanuni za Mwenendo na Miiko ya Kazi ya Uwakili kuhusu mavazi ya mawakili wanapohudhuria mbele ya Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya yatatumika kwa mawakili na wanaoendesha mashtaka katika mahakama.

Waraka wa utambulisho

8.-(1) Wakili au mwendesha mashtaka atawajibika kuwasilisha mbele ya mahakama waraka halali au ushahidi mwingine wowote unaomruhusu kuhudumu kama wakili au mwendesha mashtaka, iwapo utahitajika kufanya hivyo.

(2) Wakili au mwendesha mashtaka atakayeshindwa kutekeleza masharti ya kanuni ndogo ya (1) hatakuwa na haki ya kusikilizwa, isipokuwa kama mahakama, kwa sababu itakazoona zinafaa na kuandikwa katika mwenendo wa shauri, itaamua vinginevyo.

Ukadiriaji gharama
TS Na. 263 la Mwaka 2015

9.-(1) Ukadiriaji wa gharama za uendeshaji mashauri utakuwa kama ilivyoainishwa kati ka Amri ya Ujira wa Mawakili.

(2) Hakimu mfawidhi wa mahakama atakuwa ofisa mkadiriaji gharama chini ya masharti ya Amri ya Ujira wa Mawakili.

(3) Endapo hakimu mfawidhi siyo hakimu mkazi, hakimu mkazi yeyote aliye na cheo kikubwa zaidi katika mahakama hiyo atakuwa ofisa mkadiriaji gharama.

(4) Mhusika yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wa ofisa mkadiriaji gharama, anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio katika mahakama ya wilaya.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(3) na (4))*

### FOMU A

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya……………………………..…………
Kituo cha ………………………………………….…………
*Shauri la jinai/madai/ ndoa/ mirathi/maombi Na. ……………………………..…….
………………………………………… (mlalamikaji/mdai/mwombaji/mrufani)
Dhidi ya
…………………………………………………. (mshtakiwa/mdaiwa/mjibu maombi/mrufaniwa)
Au
Shauri la Rufaa Na. ……………………………..….
(*Kutoka Baraza la Kata la……………..katika shauri la madai/jinai Na…la 20…*)
…………………………………………. mrufani
Dhidi ya
…………………………………………………. Mrufaniwa

NOTISI YA UWAKILISHI NA AHADI YA KUHUDHURIA MAHAKAMANI

Mimi…………………, wakili wa mahakama kuu na mahakama zilizo chini yake, mwenye namba ya usajili …….. na mwenye leseni hai ya uwakili iliyotolewa tarehe……mwezi ….. mwaka 20……, ninaijulisha mahakama hii kwamba, nimeajiriwa kama wakili katika

shauri hili na nina maelekezo kamili ya (jina)……..mlalamikaji/mshtakiwa/mwombaji/mrufani/mjibu maombi/ katika shauri/ shauri tarajiwa la jinai/madai/mirathi/ndoa . Pia, ninaiahidi Mahakama kwamba nitahudhuria mahakamani kumuwakilisha ………………… katika tarehe itakayopangwa.
Saini…………………………...
Tarehe............mwezi ………………mwaka 20…….

*Futa isiyohitajika*

FOMU B

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya
ya………………………………….…………
Kituo cha …………………………………………….……………….
Shuri la jinai/rufaa/maombi Na. ……………………………..….
……………….……………………….……………. (mlalamikaji/mrufani)
Dhidi ya
……………………………….………. (mshtakiwa/mjibu maombi/mrufaniwa)
Au
Shauri la Rufaa Na. ………………………………..…….
(*Kutoka Baraza la Kata la………katika shauri la Madai/Jinai Na…la 20…*)
……………………………..…………………. Mrufani
Dhidi ya
……………………………..……………………. Mrufaniwa

NOTISI YA KUENDESHA SHAURI NA AHADI YA KUHUDHURIA MAHAKAMANI

Mimi …………………………. Mkurugenzi wa Mashtaka/Mkuu wa Mashtaka wa mkoa/wilaya …………… ninaiarifu mahakama hii kwamba, shauri la jinai/maombi/rufaa Na. ……………. la/ya mwaka ……… litaendeshwa na mwendesha mashtaka.
Pia, ninaiahidi mahakama kwamba nitahakikisha kwamba mwendesha mashtaka anahudhuria mahakamani kumwakilisha mlalamikaji/mwombaji/mjibu maombi/mrufani/mrufaniwa katika tarehe itakayopangwa.
Saini………...

Mkurugenzi wa Mashtaka/Wakili wa Serikali/Mwendesha Mashtaka wa Serikali Mfawidhi
……………………………………………………wilaya/mkoa
Tarehe...........mwezi ..………………mwaka 20……

*Futa isiyohitajika*

Dar es Salaam,
27 Februari, 2023

IBRAHIM HAMIS JUMA
*Jaji Mkuu*